
HUZUNI

# Pigo sekta ya usafirishaji ikipoteza vinara wawili



Aliyekuwa mmiliki na mwanzilishi wa kampuni ya mabasi ya Hood mkoani Morogoro, Mohamed Hood (kushoto) na mwanzilishi na mmiliki wa kampuni ya mabasi ya NBS mkoani Tabora, Nassor Hamdani (kulia), enzi za uhai wao

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Sekta ya usafirishaji wa abiria nchini imetikiswa baada ya kuwapoteza wakongwe wake wawili ndani ya siku moja, huku wadau wakisema ni pigo kubwa kutokana na mchango wao wa zaidi ya robo karne.

Wawili hao waliofariki dunia ni mwanzilishi na mmiliki wa kampuni ya mabasi ya NBS mkoani Tabora, Nassor Hamdani, na Mohamed Hood, mmiliki na mwanzilishi wa kampuni ya mabasi ya Hood mkoani Morogoro.

Hamdani alifariki dunia alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam, huku Hood akifariki dunia akiwa nyumbani kwake mtaa wa Mlapakoro, Kata ya Mji Mkuu Manispaa ya Morogoro. Wote walifariki, Februari 2, mwaka huu.

Ni wakongwe katika sekta ya usafirishaji wa abiria kwa kuwa Hamdani na Hood ni miongoni mwa wawekezaji wa mwanzo katika biashara ya mabasi ya mikoani, kabla ya kuibuka kwa kampuni nyingine nyingi zinazoonekana sasa.

Si hivyo tu, Hood ni miongoni mwa waasisi na ndiye Mwenyekiti wa kwanza wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), aliyetumikia nafasi hiyo kwa zaidi ya miaka 10, kabla ya baadaye kuachia ngazi kwa hiari.

Wadau wa sekta ya usafiri walisema vifo vyao ni pigo kubwa kwa tasnia hiyo kutokana na mchango wao katika kuimarisha huduma za usafiri wa abiria, kutoa ajira kwa Watanzania na kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Walisema kupitia uwekezaji wao, maelfu ya ajira zilitolewa kwa madereva, makondakta na mafundi, huku wananchi wakinufaika na huduma za usafiri wa uhakika, salama na wa gharama nafuu, na Serikali ikikusanya mapato kupitia kodi na tozo mbalimbali.

> "Mzee Hood na mwenzake walikuwa viongozi wa hekima na busara. Hawakupenda migogoro na Serikali, bali walipendelea mazungumzo kama njia bora ya kutatua changamoto za sekta."
>
> Katibu Mkuu Taboa, Priscus John

**Walichosema wadau**

"Mzee Hood na mwenzake walikuwa viongozi wa hekima na busara. Hawakupenda migogoro na Serikali, bali walipendelea mazungumzo kama njia bora ya kutatua changamoto za sekta," alisema Priscus John, Katibu Mkuu wa sasa wa Taboa.

Kwa mujibu wa maelezo ya John, sekta ya usafirishaji nchini imepoteza nguzo mbili muhimu za kiuchumi kutokana na vifo vyao, akisema pengo lao halitazibika kirahisi.

Alisema mzee Hood alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa mabasi ya kisasa ya Marcopolo Scania yanayofanya safari za masafa marefu, na alikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Taboa.

Alisema katika kipindi chote cha uongozi wake, Hood alihimiza wamiliki wa mabasi kushirikiana na Serikali badala ya kuchukua misimamo mikali kama migomo, akiamini mazungumzo yana tija zaidi kwa ukuaji wa biashara.

Kwa upande wa Hamdani, John alisema alikuwa miongoni mwa wawekezaji waliodumisha huduma za usafirishaji katika nyakati ngumu, hasa katika njia za vumbi kabla ya miundombinu ya barabara kuboreshwa.

"Alifanya kazi katika mazingira magumu. Njia nyingi zilikuwa hazijajengwa kwa lami, lakini aliendelea kutoa huduma hadi barabara zilipoboreshwa," alisema.

Akikumbuka mazingira waliyofanyia kazi, John alisema kipindi hicho nchi ilikuwa na kilomita chache za barabara za lami na uhaba mkubwa wa maduka ya vipuri.

"Ilikuwa kawaida basi kuharibika na kifaa cha kurekebisha kupatikana umbali wa zaidi ya kilomita 100. Wakati mwingine unakaa barabarani siku nzima. Walifanya kazi kwa jasho na damu," alisema.

Alisema wawili hao waliwekeza mabilioni ya fedha katika ununuzi wa mabasi na waliweza kuhimili soko kwa muda mrefu, jambo adimu katika sekta hiyo ambayo imekuwa ikikabiliwa na changamoto za kiafya kwa wamiliki wake, ikiwemo presha na kisukari.

"Unaponunua basi la Sh600 milioni unaambiwa faida ni kubwa, lakini uhalisia wa soko ni tofauti kabisa. Sekta hii ina changamoto nyingi zisizoonekana juu juu," alisema.

John alisema wawili hao walikuwa mstari wa mbele kupinga sera na sheria walizoziona kandamizi kwa wamiliki wa vyombo vya usafirishaji, huku wakisisitiza utoaji wa huduma bora, salama na zinazolingana na gharama halisi za uendeshaji.

"Walikuwa wakisisitiza kuwa mapato yaendane na ubora wa huduma. Walikuwa na mchango mkubwa kwa Serikali na sekta nzima ya usafirishaji," alisema.

Alisema Hamdani alikuwa nembo ya uchumi wa usafirishaji mkoani Tabora, akimiliki mabasi mengi yaliyokuwa yakihudumia ruti mbalimbali kutoka mkoani humo kwenda mikoa mingine.

John alisema sekta ya usafirishaji wa abiria ni ngumu na yenye hatari kubwa za kifedha, hali inayosababisha kampuni nyingi kufilisika ndani ya muda mfupi. Hata hivyo, Hood na Hamdani waliweza kuhimili ushindani na changamoto za soko kwa zaidi ya miaka 25.

"Walikuwa na uzoefu mkubwa na wameacha elimu muhimu kwa kizazi cha sasa cha wawekezaji. Ingawa pengo lao halitazibika, upande wa NBS kuna vijana wengi waliobaki na kampuni inaendelea kufanya vizuri," alisema.

Alisema Hood, baada ya miaka ya uwekezaji mkubwa katika mabasi, alipunguza shughuli zake katika sekta hiyo na kuelekeza mitaji katika maeneo mengine ya kiuchumi.

**Walichokisema Latra**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), Habibu Suluo, alisema taasisi hiyo imepokea kwa huzuni taarifa za vifo vya wamiliki hao wakongwe wa mabasi nchini na kwamba ni pigo kwa sekta ya usafiri na maendeleo ya uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Alisema wawekezaji hao walitoa mchango mkubwa katika kukuza sekta ya usafirishaji wa abiria, hususan kwa kuimarisha huduma za usafiri, kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania na kuchangia mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Alisema kupitia uwekezaji wao, sekta ya usafiri iliwezeshwa kuwa kichocheo muhimu cha shughuli za kiuchumi katika mikoa waliyohudumia.

"Sio familia pekee zilizopoteza, bali Taifa lote limepoteza. Latra tumepoteza, na wadau wa uchukuzi wamepoteza hazina kubwa ya uzoefu, uadilifu na uwekezaji wa wazee hawa," alisema Suluo.

Alisema mchango wao umeacha alama muhimu katika historia ya maendeleo ya sekta ya usafiri nchini, huku Latra ikiendelea kuenzi mchango wa wawekezaji hao kwa kuimarisha mazingira rafiki ya kiuchumi na kisheria yatakayochochea uwekezaji endelevu katika sekta ya usafiri.

"Tumepoteza waasisi hawa, lakini uwekezaji waliouacha utaendelea kwa kuwa ni kampuni. Hivyo pengo ni kuwapoteza wao binafsi, na tunatarajia uongozi wa kampuni zao utaendeleza uwekezaji waliouacha," alisema.

ZAIDI >

## Mbunge Tambwe afariki, kuzikwa leo

Katika hatua nyingine, aliyewahi kuwa mbunge wa viti maalumu (CCM), mkoa wa Tabora, Munde Tambwe amefariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alipokuwa akipatiwa matibabu.

Mwili wa Munde aliyewahi kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho (NEC) ulisafirishwa jana kutoka jijini Dar es Salaam kwenda Tabora na maziko yatafanyika leo, baada ya swala ya adhuhuri.

Munde aliwahi kuwa mbunge wa viti maalumu mkoa wa Tabora kwa misimu mitatu mfululizo.

Jaha Kaducha, mmoja wa wanafamilia ya Munde alisema, "Tumeondokewa na mtu muhimu kwenye familia, Munde ni zaidi ya kiongozi, mzazi na mlezi, tunamshukuru Mungu kwa zawadi ya maisha yake."



maendeleo kupitia shughuli mbalimbali zikiwamo za uchumi

# Mabasi 100 kuimarisha mwendokasi jijini Dar

**Na ATHNATH MKIRAMWENI**

SERIKALI kupitia Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), inaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha huduma ya usafiri wa umma jijini Dar es Salaam kwa kufufua jumla ya mabasi 100 yaendayo haraka kwa kuyafanyia ukarabati.

Imesema, ukarabati huo ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha huduma za usafiri wa mabasi yaendayo haraka (Mwendokasi) na kupunguza changamoto za usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, jana, Mkurugenzi Mkuu wa UDART, Pius Ng'ingo alisema mpango huo unalenga kuhakikisha mabasi yaliyokuwa yameharibika na kukaa muda mrefu bila kufanya kazi yanarejeshwa barabarani kuongeza idadi ya magari yanayotoa huduma kwa ufanisi.

Alisema katika utekelezaji wa mpango huo, baadhi ya mabasi hayo yamefanyiwa ukarabati mkubwa ikiwamo kufungwa injini mpya, hatua inayolenga kuyarejesha katika hali nzuri ya kiufundi kabla ya kuanza tena kutoa huduma.

"Hadi sasa, takribani mabasi 30 yameshafufuliwa na yako katika hatua mbalimbali za maandalizi, lengo ni kufikia mabasi 100 yanayofanya kazi bila changamoto," alisema.

Alisema mabasi hayo yaliyokarabatiwa yanachanganywa na yale yaliyokuwepo awali kuunda mfumo imara wa utoaji huduma katika awamu mbalimbali za BRT jijini Dar es Salaam.

Vilevile alisema yapo mabasi 99 mapya yaliyowasili, ambapo kuanza kwake kutoa huduma kunategemea kukamilika kwa utaratibu na miundombinu muhimu ikiwamo mifumo ya kukata nauli.

Alisema baada ya utaratibu huo kukamilika na makabidhiano kufanyika, mabasi hayo yataanza kufanya kazi bila kusubiri kwa muda mrefu.

Mabasi hayo yanatarajiwa kutoa huduma katika awamu kwa barabara ya BRT1 na BRT3, kulingana na mahitaji ya usafiri katika maeneo husika.

Ng'ingo alitaja baadhi ya njia zitakazonufaika na huduma hiyo ni Kimara, Kivukoni, Mbagala, Airport pamoja na Gongo la Mboto, ambazo ni sehemu ya mtandao wa BRT unaoendelea kuimarishwa.

Hata hivyo, kuanza kwa huduma katika baadhi ya njia, ikiwamo Airport–Gongo la Mboto, kutategemea kukabidhiwa rasmi kwa mabasi hayo.

Alifafanua kuwa, idadi ya mabasi katika kila njia itaamuliwa kulingana na uhitaji halisi wa wananchi na kwamba mpango wa kuongeza mabasi ni endelevu.

Pia, alisema wanaendelea na mpango wa biashara wa kuongeza mabasi zaidi kadri mahitaji ya usafiri yanavyoongezeka.

Alisema mpango huo unalenga kuboresha aina ya nishati inayotumika, ikiwemo kuelekea matumizi ya mabasi yanayotumia gesi, tofauti na awali.

Ng'ingo alieleza kuwa, mabasi hayo ni msaada mkubwa kwa wanafunzi na kusema yapo mabasi maalumu yanayotumika asubuhi kuwahudumia wanafunzi wanaokwenda shuleni.

Vilevile, aliwataka watumiaji wa mabasi hayo kuyatunza na kuyasimamia vizuri wakitambua ni mali ya umma yenye lengo la kurahisisha usafiri, kuunga mkono juhudi za serikali na kuchochea shughuli za kiuchumi jijini Dar es Salaam.